BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 06 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

19. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Bustani ni moja kati ya vitu muhimu sana katika kufanya mji kuwa na haiba nzuri pia hutumika kwa shughuli tofauti za kijamii na kiuchumi.

    Je, ni upi mpango wa Serikali kuiweka katika hali nzuri na stahiki

bustani ya Kiembesamaki.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

204. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na changamoto kubwa ya kupatikana mbegu za asili katika uzalishaji.

Je, Wizara inachukuwa mikakati gani kuona kwamba mbegu za asili zinapatikana na zinawatosheleza wakulima wetu.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

50. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022 imethibitisha kuwa, idadi ya wanawake ni (974,281) ambayo ni kubwa zaidi ukilinganisha na idadi ya wanaume ambayo ni (915,492).

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuwapa fursa sawa wanawake hasa katika maswali ya uongozi na ajira, ili waweze kupambana na changamoto zinazowakabili.

**Wizara ya Afya:**

145. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa tafiti zinaonyesha kuwa kinywaji maarufu cha ‘Energy Drink’ ni hatari kwa afya za wanywaji. Na kwa kuwa ripoti nyingi za kitabibu zinaonyesha kuwepo kwa ongezeko kubwa la matatizo ya moyo yanayowapata watumiaji wa kinywaji hiki sambamba na vifo vinavyoweza kuepukika, hali inayoigharimu na kuiongezea mzigo mkubwa wa matibabu Serikali.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inalifahamu tatizo hili.

(b) Je, Serikali imewahi kufanya tathmini yoyote ya kitabibu juu ya kinywaji hichi na madhara yake.

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka wa kupiga marufuku uzalishaji na utumiaji wa kinywaji hichi kwa lengo la kupunguza madhara kwa wananchi wake.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

102. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Vijiji sita (6) vya Mtangamle, Kinyuji, Fimbo, Mikirimuni, Funika na Mavuika vinapatikana katika jimbo la Mtambwe, shehia ya Mtambwe Kusini. Tangu Mapinduzi ya 1964, wananchi wa vijiji hivi hawajafikiwa na huduma yoyote ya kijamii, iwe hospitali, barabara, umeme au skuli. Wananchi hawa wamekuwa wakikabiliana na changamoto kubwa ya kufuata huduma za msingi kama afya na elimu katika maeneo ya Makongeni au Piki, ambako ni mwendo wa takribani masaa mawili kutoka vijiji hivyo, shida ambayo inakatisha ndoto za watoto wengi kwa kushindwa kufika skuli kwa kuhofia udhalilishaji.

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili kwa vijiji hivi ambavyo vinaweza kuhisi kama vimesahauliwa na Serikali yao.

(b) Je, kuna mpango gani wa haraka wa kuwapelekea wananchi hawa angalau huduma ya skuli ya maandalizi ili kupunguza umbali wa watoto wadogo kuweza kufika Piki na Makongeni.

257. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali yetu za kuboresha miundominu ya elimu, bado kuna changamoto kubwa ya uhaba wa madarasa katika skuli ya Kinowe Msingi.

(a) Vipi Serikali kupitia Wizara yako inalifahamu tatizo hili.

(b) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwatatulia wananchi hawa tatizo hili.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

127. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na tatizo la kubadilishwa kwa ratiba za meli zinazofanya safari zake baina ya Unguja na Pemba bila ya kuwataarifu wananchi na kupelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaozitegemea

meli hizo kufanya safari zao.

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hili na ni utaratibu upi hutumika wakati wa kupanga ratiba kwa meli hizi.

(b) Je, ni hatua zipi huchukuliwa kwa wamiliki wa meli hizi pindi zinapokatisha ratiba bila ya taarifa ya kutosha kwa wananchi.

(c) Je, Serikali inachukuwa hatua gani za kudhibiti na kuzuia mabadiliko ya ghafla kwenye ratiba za meli, ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa za mapema na kuondoa usumbufu.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

77. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi iliingia Mikataba na Kampuni mbali mbali kwa ajili ya utengenezaji wa boti za uvuvi zenye ukubwa wa mita 5, 7 na 8 ikiwa ni hatua moja ya utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu kwa vitendo.

(a) Je, kwa kiasi gani lengo la Serikali limefikiwa kama lilivyokusudiwa.

(b) Je, boti zilizokusudiwa mpaka sasa zimeshapatikana.

177. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

(a) Ni lini Wizara yako itaitatua changamoto ya wavuvi wetu kuvua kwa kutumia njia za kizamani.

(b) Je, utekelezaji wa wazo la wavuvi wetu la kutumia vifaa maalum vitakavyowawezesha kuona samaki kwa urahisi bila ya kubahatisha, umefikia wapi.

(c) Tathmini iko vipi juu ya maendeleo ya uvuvi kwa kutumia vifaa vya kisasa kwa wananchi waliopatiwa mkopo wa bei nafuu wa boti katika kujikomboa na umaskini kupitia uvuvi.

III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
06 Juni, 2024. KATIBU WA BARAZA